# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA AFYA
### BARAZA LA WATAALAM WA MAABARA

**Tovuti:** www.hlpc.go.tz
Simu: 0750059900

# TANGAZO

**TAREHE ZA MITIHANI YA USAJILI SEPTEMBA/OKTOBA 2025**

Ofisi ya Msajili Baraza la Wataalam wa Maabara inapenda kuwataarifu watahiniwa wote waliofanya maombi ya mtihani wa usajili kwa mwezi Septemba/Oktoba 2025 kuwa tarehe za mitihani wa usajili ni kama ifuatavyo:

| NGAZI YA ELIMU | TAREHE YA MTIHANI | | VITUO VYA MITIHANI |
|---|---|---|---|
| | NADHARIA | VITENDO | |
| **ASTASHAHADA (CMLS)** | 30.09.2025 | 01.10.2025 | KCMC, MUHAS, CUHAS MBEYA COHAS |
| **STASHAHADA (DMLS)** | 07.10.2025 | 08.10.2025 | KCMC, MUHAS, CUHAS, MBEYA COHAS, St. John's Unv Dodoma & KIUT (Kampala) |
| **SHAHADA (BMLS)** | 15.10:2025 | 16.10.2025 | KCMC, MUHAS, CUHAS MBEYA COHAS, St. John's Unv Dodoma & KIUT |

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

1. Watahiniwa wote wanatakiwa kufika katika chumba cha mtihani siku ya kwanza ya mtihani kabla ya saa 2:00 asubuhi kwa ngazi zote katika tarehe husika ya mtihani na ngazi husika. Hata kama atafanya mtihani wa vitendo pekee anatakiwa awepo siku ya mtihani wa nadharia.
2. Mtahiniwa aliyechagua kufanya mtihani kituo cha Amenye Mbeya atafanyia mtihani huo chuo cha afya Mbeya (Mbeya COHAS) kilichopo karibu na Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya. Mtahiniwa aliyechagua kituo cha UDOM atafanyia mtihani huo kituo cha *St. John's University Dodoma.*
3. Mtahiniwa wa astashahda (CMLS) ambaye kwenye mfumo kituo cha mtihani kinaonekana UDOM TAFADHALI AWASILIANE NA ofisi ya msajili kwa namba 0750059900 ili wapangiwe kituo kingine. UDOM au *St. John's University* hakuna kituo cha watahiniwa wa astashahada.
4. Kila mtahiniwa atalazimika kufika na **NYARAKA HALISI** zifuatazo kwa siku zote za mitihani;
    - Cheti cha Usajili wa awali (Provisional Registration), Koti jeupe la maabara,
    - Kitambulisho cha Serikali (NIDA, Kitambulisho cha mpiga kura, leseni ya udereva au pasi ya kusafiria). Ikiwa mtahiniwa hana kitambulisho tajwa atatakiwa kuwa na barua kutoka serikali ya mtaa ya kumtambulisha ikiwa na picha iliyogongwa muhuri
5. Mtahiniwa ambaye hatafika na nyaraka (cheti na vitambulisho) halisi **"HATARUHUSIWA KUFANYA MTIHANI".** Nyaraka laini (Soft Copy) au za kudurufu hazitakubaliwa.
6. Aidha, Watahiniwa wanakumbushwa kuwa namba za mitihani zinapatikana kwenye kwenye akaunti ya ***hprs.moh.go.tz*** ya kila mtahiniwa. Kama amefanya malipo hujapata namba ya mtihani tafadhali atuma ujumbe mfupi kwenye **0750059900**
   Ofisi ya Msajili Baraza la Wataalam wa Maabara linawatakia Mitihani mwema.

Imetolewa na
Ofisi ya Msajili
Baraza la Wataalam wa Maabara
09.09.2025

HEALTH LABORATORY PRACTITIONERS COUNCIL
09 SEP 2025
P.O.Box 743
DODOMA